

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,
S.L.P 232,
TUKUYU.
MOB- 0745774269

07/12/2020

KUMB Na. KAYSS/S. 1259/J.O/15.

JINA LA MWANAFUNZI,

.....,

S.L.P,

.....,

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARIYA KAYUKI ILIYOPO
WILAYA YARUNGWE MKOANI MBEYA KWA MWAKA 2021.**

1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanzakatika shule hii mwaka **2021**. Shule ya Sekondari Kayuki ipo umbali wa Km **10** Kusini mwa Mji wa Tukuyu kuelekea wilayani Kyela. Usafiri wa basi kutoka mjini Tukuyu Unapatikana katika kituo cha mabasi cha Tukuyu. Nauli ni Tsh **1000**. Muhula wa kuanzamasomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **10/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/01/2021**. **Muda wa kuripoti shulenii ni kati ya saa 1:30 Asubuhi hadi saa 11: 00 Jioni.**

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

- A) Sketi mbili(2) za rangi ya **dark blue** iliyokolea, mshono wa sketi-rinda box mbele na nyuma ziwe ndefu sana. Kitambaa kimeambatanishwa. Zingatia rangi na aina ya Kitambaa kilichoambatanishwa endapo kitakuwa tofauti hazitapokelewa.
- B) Sketi mbili(2) zarangi ya **damu ya mzee (kimji)** zikiwa na marinda ya kawaida (ya kufukuzana) kwaajili ya kushindia nakazi za nje.
- C) Mashati mawili(2) meupe yenyeye mikono mifupi.

- D) Sweta moja(**1**) rangi ya kijani iliyokolea.
- E) Soksi nyeupe jozi mbili(**2**), Viatu vyeusi nya ngozi vyenye visigino vifupi na nya kufunika miguu na vyenye kamba, na jozi(**1**) ya Viatu nya wazi.(sandal)
- F) Kwa wanafunzi wa Kiislamu Hijab ni nyeupe na bluu zisizokuwa na urembo
- G) T' shirt **2** za**Rangi ya Bluuzeny** kola na mistari **myeupe shingoni** na **mikononi**.

2.2 KUTOKANA NA WARAKA WA ELIMU NAMBA 6 WA MWAKA 2015
KAHUSU UTEKELEZAJI WA ELIMUMSINGI BILA MALIPO MZAZI/MLEZI
ATAKUWA NA MAJUKUMU YAFUATAYO.

- (i) Kununua sare za shule na michezo, vifaa nya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu, na chakula kwa wanafunzi wa kutwa.
- (ii) Kugharamia matibabu kwa watoto wao.
- (iii) Kulipia nauli ya kwenda Shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa na wanafunzi wa bweni wakati wa likizo.
- (iv) Kununua magodoro, shuka vifaa nya usafi binafsi kwa wanafunzi wanaosoma Shule za bweni na wanaoishi katika Hosteli zinazotumiwa na serikali, na
- (v) Kukemea na kutoa taarifa kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na elimumsingi bila malipo.

Kwa kuwa Kayuki sekondari ni shule ya hostel gherama za chakula na hostel zimeambatanishwana barua hii.

2.3 Vifaa nya Darasani:

- A) Madaftari Kumi (**10**) – Counter Books .
- B) Kalamu za wino na Risasi za kutosha (Pen na penseli).
- C) Mkebe (Mathematical set)naMathematical Table (Four Figure).
- D) Graph Paper moja.
- E) Daftari ndogo tisa (**9**) kwa ajili ya mazoezi.
- F) Karatasi za kutosha kwa ajili ya mazoezi binafsi.
- G) Jalada moja (folder file).

2.4 Mahitaji binafsi ya Bwenini:

- A) Blanketi, mashuka pea (**2**), Pea*1*we **Pink**ina pea **1** iwe **Light Blue**.
- B) Mto na Foronya ya pink na light Bluu.
- C) Ndoo 2 kwa ajili ya kuogea na kufulia.
- D) Sanduku la chuma (Trunker).
- E) Kanga mbili(**2**) au vitenge.
- F) Godoro futi 2.5 x 6.
- G) Picha nne(**4**) za passport size za rangi.
- H) Mwavuli mmoja.
- I) Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa au uthibitisho wowote wa uraia.

2.5 Chakula:

- A) Mwanafunzi anatakiwa kula chakula kinachotolewa na shule. Shule haitoi chakula maalumu na mwanafunzi haruhusiwi kujipikia au kuwa na chakula cha nyumbani.
- B) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shulenii.

2.6 Vifaa vya michezo:

- A) Track Suit moja – **Rangi ya damu ya mzee (adidas).**
- B) Raba.

2.7 Vifaa vya kazi na usafi

- A) Brash ndogo 1 ya kusugulia masinki na brash ngumu **1yenye mshikio** (Hard broom).
- B) UFagio **1wa chelewa.**

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na kama Ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. **10** ya mwaka 1995 Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI YENYE JUKUMU LA Usimamizi na Uendeshaji Elimu Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii:

- A) Heshima kwa viongozi Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- B) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- C) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparations),
- D) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa,
- E) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
- F) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,(N.B. **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUSUKA NYWELE**)
- G) Kuva sare ya shule wakati wote unapotakiwa,
- H) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
- I) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule:

- A) Wizi.
- B) Uasherati na Ushoga.
- C) Ubakaji.
- D) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi,kubeli na kadhalika.
- E) Kupigana au Kupiga
- F) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- G) Kudharau Bendera ya Taifa.
- H) Kuwa mjamzito/Kupata mimba.
- I) Kuoa au Kuolewa.
- J) Kutoa mimba.
- K) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu.

- L) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- M) Kuwa na simu ya mkononi.
- N) Kutoroka Shule au kulala nje ya Shule bila ruhusa.
- O) Kutokuwepo shulenii bila ruhusa kwa muda wa siku **30** mfululizo.
- P) Kumuliki simu.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na mwanafunzi.

- A) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii.
- B) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkatuba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- C) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 KUTOKA NJE YA SHULE:

Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule **BILA RUHUSA YA MKUU WA SHULE.**

6.0 AFYA ZA WANAFUNZI:

- 6.1 Huduma ya kwanza hutolewa shulenii kabla ya mgonjwa kumpeleka hospitalini kwa matibabuzaidi.
- 6.2 Tunaomba Mzazi/Mlezi uwe muwazi katika kutoa taarifa ya mtoto wako kuhusu hali halisi ya afya yake. Ikiwezekana vyeti vya matatizo ya kiafya kutoka kwa daktari vikabidhiwe kwa Mkuu wa Shule ili apewe huduma sahihi tatizo linapojitokeza akiwa shulenii.
- 6.3 Ni muhimu mwanafunzi awe na bima ya afya na aje nayo na kukabidhi kwa Mkuu wa shule ili imsaidie kwa matbabu ya ngazi ya juu ya shule. Mwanafunzi asiye na Bima ya afya aje nash. **6000** ili aweze kukatiwa Bima ya afya ya jamii atakayo itumia kwa mwaka **1**.
- 6.4 Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa Bwenini.
- 6.5 Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa za miti shamba shulenii.

AHSANTE.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA
KARIBU SANA SHULE YA
SEKONDARI KAYUKI.**

.....
**BERTHA. M. SARUFU
MKUU WA SHULE.**

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE.
SHULE YA SEKONDARI KAYUKI.

1. MCHANGANUO WA GHARAMA YA CHAKULA KWA KILA MWANAFUNZI.

| S/N | AINA YA CHAKULA | KIASI KWA MWANAFUNZI 1 KWA MLO | KWA SIKU | KWA WIKI | KWA MWEZI 1 | KWA MWAKA | TSH. |
|-----|--------------------|-----------------------------------|--------------------|----------------|-----------------|------------------------|------------------------|
| 1. | MCHELE | 0.25Kg | 0.25Kg | Mara 2 = 0.5Kg | 2Kg | 20Kg | @ 1950/= 39,000/= |
| 2. | MAKANDE | 0.25Kg | 0.25Kg | Mara 3=0.75Kg | 3Kg | 30Kg | @ 1000/= 30,000/= |
| 3. | MAHARAGE | 0.125Kg | 0.25Kg | Mara 14 =2Kg | 8Kg | 78Kg | @ 1900/= 148,200/= |
| 4. | UNGA (Ugali + uji) | 0.276Kg | 0.5kg | Mara 9 = 2.265 | 9Kg | 90Kg + 7kg = 97Kg | @ 1,500/= 145,500/= |
| 5. | NYAMA | 1/8 Kg | 1/8 Kg | - | Mara2 1/4 Kg | 2.5Kg | @ 5,000/= 12,500/= |
| 6. | MAFUTA | 0.0068 Lita | - | 0.0476 | 0.19 Lita | 2 Lita | @ 3,800/= 7,600/= |
| 7. | CHUMVI | 0.0051Kg | Mara 2 0.0102Kg | Mara 7 0.036 | 0.4Kg | 1.5Kg | @1,000/=1,500/= |
| 8. | KUNI | | | 2.9 | 11.6 | Mizigo 116 @ =690/= | @ 690/=80,040/= |
| 9. | MBOGA ZA MAJANI | 1/4 ya fungu @ 1= 400/= | 100/= | Mara 2 200/= | Mara 8 800/= | Mara 80 8,000/= | 8,000/= |
| 10. | MATUNDA | | | Mara 2 400/= | Mara 4 800/= | 4000/= | 4,000/= |
| 11. | VITUNGUU | 1 | | Mara 2 8.5/= | 17/= | 170/= | 170/= |
| 12. | NYANYA | | | 17 | 34 | 340/= | 340/= |
| | JUMLA | | | | | | 476,850/= |

2. GHARAMA ZA HOSTEL KWA KILA MWANAFUNZI NI TSHS 65,350/= KWA MWAKA

JUMLA KUU TSH 542,200/=

Fedha hiyo italipwa kwa awamu tatu kama ifuatavyo

- Awamu I January **200,000/=**
- Awamu II March **142,200/=**
- Awamu III July **200,000/=**

AKAUNTI NAMBA61403500098 BENKI YA NMB****

JINA LA AKAUNTI KAYUKI SECONDARY SCHOOL

N.B.Mzazi hakikisha unalipa kwa utaratibu uliowekwa na kwa wakati ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

OFISI YA RAIS

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

SIMU Na. 0732-950090
TUKUYU.

Fax.....
Kumb. Na. KAY/SS/FS/554/VOL3/



P. O. BOX 232 TUKUYU.

SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,
S. L. P. 232,

Tarehe.....

ANUANI YA MZAZI/MLEZI

.....
.....
.....
Tarehe

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,
S.L.P 232,
TUKUYU.

**YAH: HATI YA KUKUBALIMASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA
SEKONDARI YA KAYUKI.**

Mimi Mzazi/mlezi wa mwanafunzi
..... aliyekuwa akisoma shule ya msingi.....
Katika Wilaya ya
Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Kayuki ilioko Wilaya ya Rungwe kwa
kufuata masharti yafuatayo,

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida kufanya shughuli nyininge zote za shule tangu kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne, na atazingatia sheria na taratibu zote za shule.
2. Nakubali masharti na gharama zilizotolewa katika barua ya kuitwa kwa mwanafunzi (joining instructions) na nitayatimiza kwa wakati unaotakiwa.
3. Nitahakikisha atafika shulenii kwa kufuata tarehe zilizopangwa kwa kipindi chote cha miaka minne.

.....
TAREHE

.....
SAINI YA MZAZI/MLEZI

TAARIFA BINAFSI

1. Jina kamili la mwanafunzi
2. Jina kamili la mzazi

.....
Anuani kamili

.....
.....
Namba ya simu
Mkoa

3. Majina ya watatu ambao mawasiliano ya kiofisi kuhusu
mwanafunzi husika yatafanyika.

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|-------------|-----------------|----------------------|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |

4. Jina sahihi la mzazi/mlezi
JinaSahihi
5. Jina kamili la afisa mtendaji
JinaSahihi
6. Taarifa hii irudishwe kwa mkuu wa shule ya sekondari Kayuki.

.....
B. M. SARUFU
MKUU WA SHULE.

THE PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
RUNGWE DISTRICT COUNCIL

KAYUKI SECONDARY SCHOOL,

P.O. BOX 232,
TUKUYU.

TO.
MEDICAL OFFICER,
.....
.....
.....
Please examine
.....

As to her fitness for pursuing further education in this school.

1. Heamoglobin
2. P.v. Bleeding
3. Sight
4. Blood pressure
5. Urine for sugar and pregnancy tests
6. Stool routine examination
7. Asthma
8. Skin diseases
9. Leprosy
10. Epilepsy
11. Pulmonary tuberculosis
12. Deformity
13. Mental problem
14. Comments

Sign
Official stamp.